

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA

Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa, S.L.P. 28, Chamaguha, Shinyanga.  
Simu:028-2763213, Barua pepe: md@shinyangamc.go.tz, tovuti: www.shinyangamc.go.tz

**TANGAZO LA ZABUNI**

TAREHE:16.06.2021

**ZABUNI NA: LGA/112/2021-2022/NC/02.**

Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga inakaribisha maombi ya zabuni kutoka kwa Wananchi wote, Vikundi na taasisi au Mashirika yenye uwezo na sifa ya kuwa wakala wa kutoa huduma za Ulinzi na Usafi, Upangishaji mgahawa ofisi kuu, Upangishaji wa kibanda cha ATM, uwakala wa kukusanya Taka Ngumu na ushuru wa Taka Ngumu Pamoja na uwekezaji mazingira centre uliotajwa hapo chini. Ada ya zabuni ni shilingi elfu hamsini tu. (50,0000).

Maeneo yanayohitajika kuwekwa huduma hizo ni, kama ifuatavyo: -

- a) Huduma ya Usafi (Zabuni hii  
Kwa vikundi tu) - LGA/112/2021-2022/NC/01
- b) Huduma ya Ulinzi - LGA/112/2021-2022/NC/02
- c) Mgahawa ofisi kuu - LGA/112/2021-2022/NC/03
- d) Kibanda cha NMB - LGA/112/2021-2022/NC/04
- e) Mazingira Centre - LGA/112/2021-2022/NC/05
- f) Uwakala wa kukusanya Taka Ngumu na Ushuru wa taka Ngumu -  
LGA/112/2021/2022/NC/06

**Sifa za Jumla za mwombaji:**

- I. Awe na leseni hai ya biashara ya kazi husika.
- II. Awe na TIN
- III. Awe na TAX clearance" ya mwaka 2021 na kuendelea.
- IV. Awe na dhamana au mdhamini mwenye mali isiyohamishika atakayoiweka kama dhamana.
- V. Awe na ofisi yake inayotambulika
- VI. Aambatanishe uzoefu wa kazi husika.
- VII. Mwombaji awe na mkataba wa Wakala wa Huduma za Ununuzi na Ugavi Serikalini (GPSA)
- VIII. Kwa waombaji wa vikundi vya usafi waambatanishe vyeti vya usajili kutoka ofisi ya maendeleo ya jamii Manispaa ya Shinyanga.

**A: Masharti kwa mwombaji:**

- I. Aoneshe katika maombi yake kiasi cha fedha atakacholipwa/atakacholipa kila mwezi kwa zabuni atakayoomba.
- II. Maombi yafungwe kwa lakiri (seal) na yaonyeshe jina la zabuni anayoomba juu ya bahasha.
- III. Mwombaji kwa Zabuni ya Ulinzi awe na Kibali cha Kumiliki Silaha.
- IV. Mwombaji kwa Zabuni ya Ulinzi awe na Bima
- V. Awe na vitendea kazi vya kutosha kulingana na kazi husika.
- VI. Mwombaji awe na watumishi waadilifu
- VII. Mtumishi wa Halmashauri atakaye kuwa ameidhinishwa na Mkurugenzi wa Manispaa atakuwa huru kuingia katika eneo la soko au sehemu nyingine anakofanyia kazi Mzabuni wakati wowote saa za kazi kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi.

**B. Masharti ya ziada kwa wakala wa ushuru wa taka ngumu**

1. Atawajibika kukusanya taka toka kwenye maeneo ya uzalishaji (kaya, taasisi na biashara mbalimbali) na kupeleka moja kwa moja kwenye Dampo Kuu Nhelegani.
2. Atawajibika kukusanya ushuru wa taka kwa viwango vilivyoainishwa kwenye Sheria ndogo ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga (Usafi wa Mazingira) ya mwaka 2014 kama ilivyofanyiwa marekebisha (ada na ushuru ) mwaka 2019
3. Atawajibika kukusanya Ada ya taka kwa kutumia mashine ya kielektroniki.


**C. Masharti ya ziada kwa atakayepewa zabuni ya kuendesha mgahawa Ofisi kuu:**

- I. Atawajibika kulipa gharama za maji na umeme
- II. Aoneshe katika maombi yake kiasi cha fedha atakacholipa kila mwezi kwa zabuni ya kuendesha mgahawa.

Maombi yote yatumwe kwa: -

**KATIBU WA BODI YA ZABUNI,  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA,  
S.L.P. 28, SHINYANGA.**

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **30/06/2021** saa **4:00** asubuhi. Zabuni zitafunguliwa siku hiyo hiyo. Waombaji mnakaribishwa kuhudhuria sherehe za ufunguzi.



Geoffrey R. Mwangulumbi  
**MKURUGENZI  
HALMASHAURI YA MANISPAA  
SHINYANGA**

**Nakala:**

**Katibu Tawala (M)  
S.L.P 320  
Shinyanga**

**Katibu Tawala (W)  
S.L.P 320  
Shinyanga**

**Mbao zote za Matangazo  
Halmashauri ya manispaa ya  
Shinyanga.  
Halmashauri zote za Mkoa wa Shinyanga.**